

# Ripoti ya jambo linaloshukiwa (SMRs)

## Taarifa muhimu kwa watoa huduma za kifedha

### Ripoti ya jambo linaloshukiwa ni nini?

Ripoti ya jambo linaloshukiwa, au SMR, ni ripoti ambayo lazima uwasilishe kwa AUSTRAC wakati wowote unapokua na shaka juu ya mteja au muamala.

Lazima uwasilishe SMR ikiwa una shaka kuwa shughuli hiyo inaweza kuhusishwa na ufadhili wa ugaidi, utakatishaji fedha, au sheria yoyote ya Jumuiya ya Madola, jimbo au wilaya, hata ikiwa huna hakika kuwa uhalifu unafanywa.

Lazima pia uripoti jambo unalotilia shaka kwa AUSTRAC hata ikiwa hautaishia kutoa huduma au hata ikiwa mteja ameuliza jambo lenye mashaka.

### Kwanini ni muhimu kuripoti SMRs?

SMRs husaidia AUSTRAC na washirika wetu (ikijumuisha mawakala wa utekelezaji wa sheria) kuchunguza na kuzuia uhalifu mkubwa. SMR yako inaweza kuwa kipande kwenye fumbo ambalo husaidia kuzuia uhalifu.

SMR yako inaweza kujumuisha taarifa muhimu ambayo inaweza kusaidia uchunguzi wa jinai wa sasa au kusaidia kutambua, kuzuia au kuvuruga shughuli za jinai.

Kwa kuripoti SMRs, unasaidia kuilinda biashara yako na jamii dhidi ya uhalifu.

### Wakati na jinsi ya kuripoti SMRs

Lazima uwasilishe SMR:

- Ndani ya masaa 24 ya kuwa na shaka inayohusiana na ufadhili wa ugaidi
- Ndani ya siku tatu za kuunda tuhuma inayohusiana na jambo lingine lolote.

### Usahihi wa SMRs

Usahihi wa SMR zako utaokoa muda wako wa biashara na pia kuhakikisha AUSTRAC inapokea taarifa muhimu zinazoweza kutumiwa na watekelezaji wa sheria na mashirika ya washirika kuvuruga shughuli za uhalifu. Hapa kuna vidokezo muhimu vyta kuhakikisha SMRs zako zinatoa taarifa bora.

### FANYA

- ✓ Eleza kile unachofikiria kinatokea mbele. Tuambie kwa nini una mashaka katika aya ya kwanza, kisha toa maelezo zaidi juu ya wahusika na shughuli zinazohusiana na mashaka yako. Kuwa muwazi na kwa ufupi.
- ✓ Eleza kile kisicho kawaida katika shughuli inayoripotiwa.
- ✓ Ongeza taarifa na muktadha wa ziada. Mashaka yako yanaweza kuwa yanahusiana na muamala huo, lakini pia mashaka yanaweza kuhusiana na tabia na uchunguzi. Jumuisha uchunguzi wako juu ya tabia ya mteja, na mwonekano ikiwa ni muhimu.
- ✓ umuisha viunganishi vyovyyote husika kati ya vyombo vinavyoripotiwa na wateja wengine. Kwa mfano ndugu wa familia au washirika wa biashara.
- ✓ Kuwa sahihi na tahajia, anwani, tarehe za kuzaliwa na maelezo ya kitambulisho.
- ✓ Ingawa haionekani kila wakati, tafadhali toa makisio yako juu ya kosa linaloshukiwa kuwa limetendwa.

## USIFANYE

- ✗ Jumuisha habari inayorudiwa juu ya vyombo au shughuli.
- ✗ Kutoa msingi mrefu wa mashaka (GFS). Weka wazi na kwa ufupi.
- ✗ Kuambatisha vibali au notisi kutoka kwa watekelezaji sheria na wakala wa serikali au picha zisizofaa.
- ✗ Kujumuisha maelezo yasiyo ya lazima ya biashara ambazo zinajulikana sana au hutafutwa kwa urahisi.
- ✗ Kujumuisha majina au mawasiliano ya maafisa wa polisi au wafanyakazi katika sehemu ya GFS.

## USISAHAU

- Kwa sheria, SMRs unazotoa zinahifadhiwa kwa siri na AUSTRAC na mashirika yetu ya washirika. SMR haikubaliki kama ushahidi kortini au vikao vya mahakama.
- Isipokuwa ni jambo linalohitaji kuhusisha watekelezaji wa sheria, usimwambie mtu yeyote isipokuwa AUSTRAC kwamba umetia shaka juu ya mteja au kwamba umewasilisha SMR. Kinyume chake, ikiwa umeripoti polisi, kuna uwezekano unahitaji pia kuripoti suala hilo kwa AUSTRAC.
- Lazima uwe na busara unapotafuta taarifa zaidi kutoka kwa mshukiwa ili kuepuwa kumtahadharisha. Kumtahadharisha kunaweza kufanya iwe ngumu kwa watekelezaji wa sheria kuchunguza shughuli za uhalifu.
- Pitia michakato ya biashara yako mara kwa mara ili kuhakikisha ina uwezo wa kutambua shughuli zozote zinazotiliwa shaka.
- Kuwasilisha SMRs hakutasababisha AUSTRAC kuona biashara yako vibaya. Kuripoti kunaonyesha kuwa una mfumo dhabiti wa ufuatiliaji na mpango wa AML / CTF.
- Ikiwezekana, jumuisha picha zozote zinazofaa za CCTV, anwani za IP au picha kama viambatisho kwenye mawasilisho yako ya SMR.
- Rejelea wavuti ya AUSTRAC na akaunti yako ya myandaoni ya AUSTRAC kwa rasilimali zaidi.

